

**IDARA YA HAKI ZA KIBINADAMU YA IOWA  
KITENGO CHA MAWAKALA WA SHUGHULI ZA KIJAMII**

**PROGRAMU YA USAIDIZI WA KAWI YA NYUMBANI KWA WAKAZI WENYE MAPATO YA CHINI  
UTARATIBU WA RUFAA NA USIKILIZWAJI**

Mwombaji anaweza kuanzisha utaratibu wa kuomba rufaa iwapo ombi hilo lilikuwa limekataliwa awali, ama ukweli halisi au utaratibu usiofaa ulitumika ili kutoa maamuzi ya ustahiki, kiwango cha fedha cha usaidizi, ama huduma. Mwombaji ana siku 30 za kalenda kuanzia tarehe ya uidhinishwaji ama barua ya ukataliwaji wa ombi la rufaa ya maamuzi kwa kutuma baruapepe ama kulifikisha ombi hilo kwa afisi ya wakala wenyeji anayesimamia (LAA) kituo ambacho ombi hilo lilitumwa.

Iwapo LAA ima itaidhinisha au kukataaombi hilo ndani ya kipindi cha siku 30 za kalenda baada ya kupokea ombi kamili, mwombaji huyo anaweza kuchukulia kwamba hali hiyo ya kutoshughulikiwa kwa ombi ni sawa na maamuzi ya ombi kukataliwa. Kisha mwombaji ana siku 30 za ziada za kutuma rufaa.

Ili kutuma rufaa, mwombaji (mdai) ni lazima atume rufaa kwa maandishi kwenda kwa LAA ilipotumika, na kuhusisha hatua ambayo mwombaji angependa ichukuliwe, na taarifa nyingine yoyote ambayo inaweza kuathiri maamuzi hayo. Wadai hao ambao hawajui kusoma ama kuandika, watasaidiwa na LAA katika kusoma, kuandika, ama kuelewa vyema rufaa hizo, kuitikia kesi, na taratibu nyinginezo zinazohusiana shughuli hiyo.

LAA itashughulikia ombi la mdai na kumfahamisha mdai matokeo ya ombi kwa maandishi ndani ya siku saba za kalenda kuanzia tarehe ombi hilo lilipotumwa (wekea alama tarehe hiyo iwapo ilitumwa kwenye baruapepe).

Ikiwa mdai hakubaliani na maamuzi yaliyotolewa, mdai huyo anaweza kuandika barua kwa LAA ndani ya siku 14 za kalenda baada ya maamuzi (wekea alama tarehe hiyo iwapo ilitumwa kwenye baruapepe) na kisha aombe kwamba kesi hiyo isikilizwe na Kitengo cha Mawakala wa Shughuli za Kijamii (DCAA). Mdai ni lazima aelezee kwa maandishi ni kwa ni i maamuzi ya wakala yanafanyiwa rufaa na pia ahusishe taarifa yoyote inayoweza kuathiri maamuzi.

LAA itatuma taarifa yote kuhusu ombi hilo la kusikilizwa kwa kesi kwa DCAA na usikilizwaji huo wa kesi utawekewa tarehe ndani ya siku 14 za kalenda baada ya kupokea rufaa pamoja na ombi kusikilizwa kwa rufaa hiyo. Mdai atapokea ilani iliyoandikwa ya tarehe ya kusikilizwa kutoka kwa kitengo hicho. Ilani hiyo itaonyesha tarehe, muda, na sehemu itakaposikilizwa rufaa hiyo. Usikilizwaji huo wa jimbo unaweza kufanyika kupitia kwa simu kwa muda uliokubalika kwa pande zote husika ama ana kwa ana. Wakati wa kusikilizwa kwa rufaa, taarifa zote zitatathminiwa na maamuzi yatatolewa na kitengo hicho ndani ya kipindi cha siku 7 za kalenda.

Mteja huyo anaweza kutuma rufaa ya maamuzi hayo ya DCAA kwa Idara ya Ukaguzi na Rufaa ya Iowa (DIA). Mteja ni lazima atume rufaa kwa maandishi kwa DCAA ndani ya siku 7 za kalenda (wekea alama tarehe hiyo iwapo ilitumwa kwenye baruapepe) baada ya kupotea maamuzi ya kitengo hicho cha DCAA. Maamuzi hayo yatafuata taratibu za rufaa zilizowekwa katika sehemu ya 481 ya Sura ya 10 ya Msimbo wa Kiutawala wa Jimbo la Iowa.